**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE**
**BANGOKITITA LA MPANGO WA MATOKEO YA MABORESHO YA MAZINGIRA YA BIASHARA KATIKA SERIKALI ZA MITAA (LBER)**

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kurahisisha usajili wa biashara na utoaji leseni | • Kuongeza biashara zilizosajiliwa kutoka 300 hadi 500 kufikia Juni, 2019<br>• Kuongeza mapato yanayotoka na na leseni kutoka Tsh. 24,000,0000/= hadi Tsh. 30,000,000/= kufikia Juni, 2019 | • Kufanya vikao vya kuelimisha watu kuhusu usajili wa biashara na utoaji leseni katika maeneo ya Munanila, Kinazi Muyama, Buhigwe na Janda<br>• Kumuagiza Mtendaji wa Kijiji kuacha kudai malipo ya kusaini barua za utambulisho za TRA<br>• Kutoa vifaa muhimu vya kuanzisha OsBC na kuhakikisha kuwa huduma zote zinapatikana katika eneo moja. | ➢ Kuanzishwa kwa biashara mpya 200<br>➢ Ongezeko la mapato yanayotokana na leseni za biashara kwa Tsh.6,000,000/= | ➢ Ongezeko la mapato yanayoto kana na leseni za biashara kwa Tsh. 6,000,000/=<br>➢ Kupatiwa mafunzo kwa watumishi 20 kuhusu matumizi ya POS.<br>➢ Biashara mpya kusajiliwandani ya siku 3<br>➢ Taasisi tano (Mamlakaya Biashara, | ➢ Kuanzishwa kwa biashara mpya 200<br>➢ Biashara mpya kusajiliwa ndaniya siku 3 |

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | TRA, BRELA, Mabenki na SUMATRA) kufanya kazi pamoja katika OsBC. | |
| 2 | Kuunganisha kodi, ushuru na tozo mbalimbali ili kupunguza kodi zinazofanana | Uanzishwaji wa kodi moja | • Kufanyika tafiti za kubaini kodi, ushuru na tozo mbalimbali zinazofanana na kubainisha namna bora ya kuziunganisha au kuziondoa kama vile kodi ya zuio n.k<br>• Kubuni na kutekeleza programu za elimu kwa umma kuhusu ulipaji kodi kwa lengo la kuongeza ufahamu wa ulipaji kodi na umuhimu wake katika jamii.. | Kuwepo kwa namna moja ya ulipaji kodi | ➢ Kuanzishana mna moja ya ulipaji kodi | ➢ Kuwepo kwa mfumo wa kusawazisha viwango vya kodi, ushuru na tozo |

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Kuwezesha/Kurahisisha biashara za mpakani (nchi jirani) | • Kuongeza idadi ya wafanyabiashara katika nchi za jirani kutoka 200 mpaka 300 kufikia Juni, 2019<br>• Kuongeza masoko ya nchi jirani kutoka soko 1 hadi 3 kufikia Juni, 2019 | • Kuwaelimisha wadau kuhusu namna ya kuzichangamkia fursa za biashara za nchi jirani<br>• Kuzitangaza fursa za biashara zinazopatikana katika nchi jirani<br>• Kuongeza ushiriki wa jamii katika biashara za nchi jirani<br>• Kufanyika kwa vikao vya robo mwaka vinavyoshirikisha Halamashauri ya Buhigwena nchi ya Burundi kuhusu biashara za nchi jirani/mpakani<br>• Kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara (wa kike na wakiume) | • Ongezeko la wafanyabiashara 100 kwa mwaka wanaojihusisha na biashara za nchi jirani<br>• Kuanzishwa kwa soko jipya la Kilelema na Kibande<br>• Kuongezeka kwa bidhaa mpya zinazouzwa katika biashara za nchi ya jirani | ➢ Ongezeko la mapato ya Halmashauri kwa Tsh. 50,000,000/=<br>➢ Tani 5,000 za bidhaa kuuzwa katika biashara za nchi jirani | ➢ Ongezeko la wafanyabishara 100 kwa mwaka<br>➢ Kuanzishwa kwa soko jipya la Kilelema na Kibande |

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | yanayohusiana na masoko ya kimataifa.<br>• Kutenga bajeti ya ujenzi wa masoko. | | | |
| 4 | Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika uundaji wa sera mpya | Ongezeko la wadau kutoka sekta binafsi katika vikao vya kanseli kutoka washiriki 0 hadi 3 kufika Juni, 2019 | • Kualikwa kwa wadau wa sekta binafsi katika vikao vya kanseli<br>• Kufanyika kwa vikao vya wadau wote | • Kushiriki kwa wadau 3 wa sekta binafsi katika vikao vya kanseli | ➢ Kufanyikakwa vikao vine vya Baraza la Biashara la Wilaya DBC kwa mwaka<br>➢ Kuandaliwa kwa muhtasariwa vikao na ripoti mbalimbali<br>➢ Ushiriki wa wadau kutoka sekta binafsi | ➢ Kuimarika kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uandaaji wa sera kupitia vikao vya kanseli |
| 5 | Kuimarisha upatikanaji wa ardhi/maeneo ya uwekezaji | Ongezeko la maeneo ya uwekezaji kutoka viwanja 100 hadi 300 kufikia Juni, | • Upimaji na utoaji ramani katika viwanja 300<br>• Kufanya warsha kuhusu Sheria ya | • Kutengwa kwa viwanja 200 kwa ajili ya uwekezaji | | |

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2019 | Ardhi Na.4 na 5 ya mwaka 1999 na kufafanua namna ya kupata Hati za Kimila (CCROs) hasa kwa wanawake ambao ni kundi maalumu linalotengwa katika jamii | • Kuongezeka kwa idadi ya wamiliki wa viwanja vya uwekezaji | | |
| 6 | Kuimarisha mazingira ya kibiashara | • Ongezeko la leseni za kibiashara kutoka leseni 300 hadi 400 kufikia Juni 2019<br>• Kupungua kwa siku za kuomba hadi kupatiwa leseni | • Kutambua na kurasimisha biashara<br>• Elimu kwa umma<br>• Kusajili biashara<br>• Kuanzisha kituo kimoja ambacho huduma zote za usajili wa biashara hupatikana (*One Stop Business Centre*)<br>• Kutengwa bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya | • Idadi ya biashara zilizosajiliwa na kupatiwa leseni<br>• Kupungua kwa idadi ya siku za kusubiria kukamilika kwa usajili wa biashara mpya na kupatiwa leseni | • Kusajiliwakwa biashara mpya 10<br>• Usajili wa biashara mpya ndani ya siku 2 | • Usajili wa biashara mpya ndani ya siku 2 |

| Na. | Malengo Mkakati | Matarajio | Mipango | ViashiriaMuhimu | Viashiria vya Mafanikio | Viashiria vya Matokeo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | kutoka siku 7 hadi 2 kufikia Juni, 2019. | biashara | | | |
| | | Kupunguzwa kwa vituo vya ukaguzi vya barabarani kutoka 4 hadi 2 kufikia Juni, 2019 | • Kushirikiana na polisi pamoja na kuwafahamisha umuhimu wa kupunguza vituo vya ukaguzi barabarani kwa minajili ya kuchochea mazingira ya kibiashara | • Kupunguzwa kwa vituo vya ukaguzi barabarani | • Kupunguzwa kwa vituo viwili vya ukaguzi barabarani | |